ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

		na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake

29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake

86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 8 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika Mkutano wa Nane wa Baraza la Tisa la Wawakilishi katika kikao cha Tarehe 12 Disemba, 2017 Mhe. Mussa Foum Mussa aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, wakati najibu swali Nam. 26 niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Mussa Foum Mussa aliyetaka kujua ni watu wangapi walioanguka katika mikarafuu kwa mara hii Unguja na Pemba na je, watalipwa haki yao ya kuanguka. Jibu la swali hili ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mwaka huu jumla ya wakulima 175 wameripotiwa kuanguka katika mikarafuu ambapo kati hao wakulima 167 wameanguka katika mikarafuu kwa upande wa Pemba na wanane (8) kwa upande wa Unguja. Vile vile wakulima hao wanatarajiwa kulipwa haki zao baada ya kukamilika utaratibu. Mhe. Spika, ahsante.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 28

Honi Wakati wa Kuanza na Kumaliza Muda wa Kazi na Magharibi

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar wamezoea honi ikilia wakati wa asubuhi, saa moja na nusu, saa tisa na nusu, na magharibi.

(a) Je, hatuoni kuwa kupiga honi kwa sasa inawezekana kuwa matumizi yake hayahitajiki kama ilivyokuwa yakihitajika zamani kwa kuwa kila mmoja anayo saa au simu.

(b) Kwa kuwa matumizi ya honi hutumika duniani ikiashiria hali ya hatari au maafa, Je, hatuoni kuwa tunawashtua wageni wanaotembelea visiwa vyetu.

(c) Ni kwanini matumizi ya honi hayatumiki katika mikoa mingine pamoja na Pemba ili dhamira yake kuu ikajulikana na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutanguliza maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, matumizi ya huduma ya honi yalianza kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 na imekuwa ikiendelea hadi

leo hii bila ya athari yoyote katika jamii yetu. Lengo la huduma hii ni pamoja na kuashiria kuanza kwa muda wa kufanya kazi yaani saa 1:30 za asubuhi, kutoka kazini yaani saa 9:30 za laasiri, na kupandisha na kushushwa kwa bendera wakati wa magharibi, pamoja na kuashiria hali isiyokuwa ya kawaida pale inapojitokeza.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika**,** serikali bado inaona ipo haja ya matumizi ya honi hii kwani madhumuni ya kuanzishwa kwake bado yanaendelea licha ya kuwepo kwa maendeleo ya teknolojia ya habari.

(b) Mhe. Spika, wageni wote wanapoingia nchini hupewa taarifa zote muhimu za mazingira ya nchi na utamaduni wa Uzanzibari, na hadi sasa hakuna malalamiko yoyote yaliyoripotiwa kutoka kwa wageni wanaoitembelea Zanzibar kwamba wamepata mshtuko au mfadhaiko uliosababishwa na uliaji wa honi.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya utangulizi kwamba tumekuwa na utamaduni wa kutoa huduma hii ya honi katika maeneo ya mjini tu. Hatua hii imetokana na maeneo hayo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu pamoja na huduma mbali mbali za kijamii na kiserikali zinatolewa kwa wingi. Serikali kwa sasa bado haijapanga kuweka huduma ya honi katika maeneo mengine ya nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikiri mimi ni mfuasi mkubwa na naipenda sana honi.

Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilikuwa namuuliza swali moja tu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, katika dunia ya sasa ukiangalia dhana kuu ya honi ni kuashiria hali ya hatari hasa katika maeneo ya Visiwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kutokana na aidha mambo yaliyotokezea kama kule Japan ilipotokea SUNAMI na Mwenyezi Mungu atuepushe. Lakini pia pale panahitajika kutoa ishara kama ni *curfew*. Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni umuhimu kwamba ili kuhakikisha wananchi hasa na wageni pia wanaoingia Zanzibar wanaondokana na mshtuko huu. Ni utaratibu upi serikali inachukua kuhakikisha kwamba pale wageni wanapoingia katika njia mbili kuu za Bandarini na *Airport* wanapata taarifa kamili pamoja na mahoteli wanapofikia.

Lakini (b) katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba pamoja na huduma mbali mbali za kijamii zinazotolewa na serikali kwa wingi ni hasa katika Mkoa wa Mjini. Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni umuhimu wa honi hii kuwepo Pemba pia au Pemba sio mji.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi , Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Naomba nianze na (b). Mhe. Spika, kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi utaratibu wa kupiga honi huu umewekwa katika miji ambayo kuna shughuli nyingi rasmi za Kiserikali. Lakini utamaduni wa kufanya matukio kama hayo mara nyingi katika nchi na Mataifa mengi tofauti utamaduni huu unakuwepo katika ile Miji Mikuu na Makao Makuu ya nchi. Sasa kwa mazingira yetu ya Zanzibar tulipozungumzia Mkoa wa Mjini

Magharibi unabeba mikoa mingine yote mitano (5) iliyokuwepo. Kama shughuli nyingi za Makao Makuu ya nchi yapo hapa ina maana *symbol* kinachofanyika hapa kinaashiria jambo lile kufanyiwa utekelezaji katika mikoa mingine. Kwa hiyo hili jambo Mhe. Spika, lipo hata duniani kote katika nchi tofauti tunapotaja mji mkuu au makao makuu ya nchi kunakuwa kuna sifa za pekee ambazo zinaashiria kuna tukio linalofanyika pale linatakiwa liende sambamba na mikoa mingine.

Lakini pia swali lake la (a) kwamba vipi tunaweza kutoa taarifa hizi hasa kwa wageni pale wanapoingia hasa katika *entry point* zetu zile za *Airport* na Bandarini. Jambo hili limekuwa likifanywa na mara nyingi kuna taasisi za *Tour* ambazo zimekuwa na utamaduni wa kujua hali yote ya mazingira ya kwetu wenzetu hawa wanafanya. Hata yeye Mhe. Simai Mohammed Said tunafahamu jambo hili kupitia zile taasisi zao za Utalii wamekuwa wakifanya jitihada kubwa sana za kuwaelimisha na kuwatanabahisha hali halisi ya watalii wote ilivyo, hali halisi ya mazingira yetu muda fulani, ile silka na asili ya Uzanzibari wamekuwa wakiambiwa wageni wetu na hili ni jambo la urithi kwetu.

Bahati nzuri leo tu imeonekana kidogo nidhamu imepungua maana wakati huo baada ya Mapinduzi ilipokuwa ikipigwa honi kama asubuhi au saa 12:30 za jioni wakati wa kushusha bendera heshima ilikuwa nidhamu kwamba mtu popote pale alipo honi anapoisikia ilikuwa anastahiki na ana wajibu wa kusimama kuashiriwa kushushwa kwa bendera. Hichi ndicho kitu ambacho kimekuwa kikifanyika. Tuendelee kuwaomba sana Wazanzibari wote kwa ujumla turudishe nidhamu yetu kama ilivyokuwepo hapo awali baada ya Sherehe za Mapinduzi. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kuipongeza serikali kwa kuendeleza utamaduni wa kuliza honi, ninaamini kuliza honi huku ni kuendeleza Mapinduzi Matukufu yaliyoasisiwa tarehe 12 Januari, 1964.

Mhe. Spika, pia napenda kuipongeza serikali kwamba kila nchi ina utamaduni wake. Unapokwenda China ilikuwa ukipita pale kwa *Chairman Mao* lazima upige saluti kwa sababu yule ni muasisi na kwa maana ya kuyalinda Mapinduzi ya Kichina. Kwa hiyo, naipongeza serikali kwa kuyaendeleza na kuyalinda Mapinduzi kwa kuliza honi katika mkoa huu wa mjini.

Mhe. Spika, swali langu ni kwamba zamani ilikuwa inapolia honi tunasimama. Je, ni lini serikali itarudisha utamaduni ule wa kisheria na kisera kwamba inapolia honi watu wasimame.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi , Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh, rafiki yangu, ndugu yangu, jirani yangu swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama ambavyo nimejaribu kutoa maelezo katika jibu langu la msingi kwamba hapo awali baada ya Mapinduzi tumerithi utamaduni mkuu uliokuwa ukiashiria mambo mengi, lakini wakati ule watu wa Zanzibar walikuwa na nidhamu ya hali ya juu. Kweli katika miaka ya leo hatujajua kama ni utandawazi wa teknolojia ama ni kukua kwa baadhi ya mambo na kubadilika. Lakini tunakuwa tunawaomba jambo la kwanza jamii serikali tutakuja kutoa utaratibu katika siku zijazo kutoa maelekezo wakati wa kupigwa honi asubuhi, saa 9:30 na saa 12:30, hata pale

itakapotokea jambo lolote la hatari tutatoa utaratibu maalum na utatangazwa rasmi. Lakini kwa sasa tuendelee kuwaomba Wazanzibari wote kwa jumla turudi katika utamaduni tuliokuwa tukiufanya baada ya Mapinduzi yetu ya mwaka 1964 hilo ndio jambo la msingi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nimefurahia majibu ya Waziri kwa heshima ambayo ameirudisha katika nchi yetu. Mhe. Spika, swali langu lenye vipengele (a) na (b) linakuja kwamba kwa sasa hivi mji mkuu nambari mbili ni mji wa Chake Chake umekuwa kwa kasi au ni mji mkuu. Hili jambo la honi alisema Mhe. Waziri kwamba ni la miji mikuu na kile ni kisiwa chengine sio kisiwa kile kile. Je, ni lini Chake Chake atatupatia honi ili na sisi tutakapokuwa tunakuja Zanzibar tuwe tunafahamu heshima ya honi isijekuwa wengine wamesimama wengine wanakwenda.

Lakini swali (b) katika muendelezo wa masuala haya pia kama neno la heshima pia na sisi kule Pemba tunahitaji heshima ya honi. Kwa hiyo, ni lini atatupatia honi Chake Chake ili kila mmoja afahamu hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi , Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said maswali yake yote kwa pamoja (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mimi narudi pale pale, mji mkuu wetu ni Mkoa wa Mjini Magharibi kwa Visiwa vya Unguja na Pemba, maana tuna visiwa vya Tumbatu, Fundo vyote ni visiwa. Lakini tunapozungumzia Mji Mkuu ni Mkoa wa Mjini Magharibi *concern* yake kwamba kuhamishia Chake Chake kwa upande wa Pemba kwenda kupiga honi hatukatai kama serikali tunapokea

tutatizama kwa kina shauri hilo, itakapobidi tutafanya jambo hilo kwa sababu ni utamaduni ambao unapaswa kuendelezwa katika kila sehemu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 5

Mpango wa Kuimarisha Wana *Diaspora*

Mhe. Miraji Khamis Mussa - Aliuliza:

Katika moja ya tukio muhimu la kihistoria na lenye maslahi kwa nchi ya Zanzibar ni kufanyika kwa mkutano mkubwa wa tatu wa wana *diaspora* mwishoni mwa mwezi Agosti, 2016 ambao ulifunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein.

(a) Je, Sera ya *Diaspora* imefikia wapi katika kuunganisha malengo mazuri yaliyopatikana kwenye mkutano wa wana *diaspora* uliofanyika Zanzibar.

(b) Kwa kuwa wana *diaspora* wamekosa kiunganishi kizuri. Serikali ina utaratibu gani wa kuwaunganisha wana *diaspora*.

(c) Kwa kuwa serikali ilichukua jitihada nzuri za kuwatambua wana *diaspora* kote duniani. Ni wana *diaspora* wangapi ambao serikali imeweza kuwatambua na kukaa nao na kuwaeleza azma ya serikali ya kuanzisha Idara ya *Diaspora*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeipitisha Sera ya *Diaspora* ya Zanzibar na kuagiza utekelezaji wake tokea mwezi Julai, 2017. Hatua zinazoendelea hivi sasa ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuitangaza sera hiyo pamoja na kukutana na wahusika wote ili kurahisisha utelekezaji wake. Jambo hilo litafanyika katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

(b) Mhe. Spika, sio kweli kwamba wana *diaspora* wanakosa kiunganishi kizuri katika kuwaunganisha kati yao na serikali. Moja kati ya kiunganishi kikubwa ni uwepo wa Idara Maalum katika serikali inayoshughulikia na masuala ya *diaspora*. Aidha, kwa takriban kipindi cha miaka minne tumekuwa tukiandaa makongamano haya kama jukwaa zuri la kubadilishana mawazo kati ya serikali na *diaspora*. Ni imani yetu kwamba Ofisi zetu za Kibalozi nje ya nchi na Asasi/Jumuiya za *Diaspora* za Kikanda, tutaendelea kuimarisha mahusiano yetu. Upatikanaji wa Sera hii ya *Diaspora* Zanzibar ndio uthibitisho tosha wa utayari wa serikali katika kushirikiana na wenzetu hao *diaspora*.

(c) Mhe. Spika, kwa sasa idadi kamili ya wana *diaspora* wa Zanzibar bado haijafahamika. Hata hivyo, serikali inafanya juhudi za kuwatambua na kuwasajili wana *diaspora* kupitia idara yetu. Kwa upande wa Jumuiya za wana *Diaspora* serikali inashirikiana nazo ni Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nchi za Scandinavia *(ZANDIAS)*, Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi Canada *(ZACADIA)*, Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi Marekani *(DICOTEA)*, Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi Maryland *Marekani (HEAD INC)*, Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nchini Uingereza *(ZAWA)* na Jumuiya ya Wazanzibari anaoishi

Birmingham nchini Uingereza na miji mingine, pamoja na Mashariki ya Kati na Asia.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, nataka nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake marefu lakini ndani yake yakawa yanapishana hivi. Mhe. Waziri katika majibu yako huwezi kukaa na Idara inayofanya kazi kwa kipindi cha miaka minne (4) kama ulivyokiri mwenyewe halafu suala la idadi ya utambuzi kwa wana Diaspora ikawa mpaka muda huu jibu lako maana yake huwajui.

Swali (a) je, Wizara yako inatoa ahadi gani katika zoezi la utambuzi wa wana *diaspora* ili kuweka sawa utaratibu wa kuwajua baadhi ya wataalam ambao wanatokana na kundi hilo la wana *diaspora*.

Swali (b) Mhe. Waziri umesema swali la kuitangaza sera liko katika mwaka huu wa fedha. Je, ni shughuli gani mlizozipanga katika utekelezaji wa kuitangaza sera hiyo. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa maswali yake mawili (2) ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, swali la kuitambua idadi ya wana *diaspora* naomba nichukue nafasi hii kujaribu kueleza kipi ambacho *diaspora* wapo na kwa kiasi gani sisi tunashindwa kuwatambua idadi yao. Pia hoja ya Mhe. Mjumbe kwamba kwa kipindi cha miaka minne (4) Idara ipo kwa nini wameshindwa kuitambua idadi halisi ya wana *diaspora*.

Mhe. Spika, sote tunajua kwamba tutakapotoka katika mipaka ya Tanzania maana yake hakutakuwa na Mzanzibari kwa utaifa wake, sote tunabakia kuwa na sera kwa maana kwamba *diaspora* atajulikana kama Mtanzania. Watanzania hawa wanapokuwepo huko sisi idara yetu tunachokifanya ni kushirikiana na Taasisi nyengine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwemo Balozi, Idara husika inayoshughulika na wana *Diaspora* na Taasisi nyengine ili kuweza kuwabaini Watanzania hao na wale wenye asili ya Zanzibar, ndipo tutaweza kujua idadi yake. Lakini sote tunajua tunao watu ambao wameondoka Zanzibar kwa nyakati tofauti wapo wanaendelea kukubali kwamba wao ni Watanzania na wapo ambao wameendelea kukataa kama wao si Watanzania.

Kwa hiyo, wajibu wetu sisi kushajihisha mahusiano mazuri. Ninachoshukuru kwamba wapo *diaspora* ambao wao wenyewe kwa kushirikiana na serikali wameanzisha jumuiya zao kwetu sisi kwa kupitia jumuia inakuwa rahisi sana kuweza kutambua idadi yao. Lakini wale ambao hawajajihusisha kupeleka taarifa zao katika jumuiya zao itaendelea kutuwia vigumu kuweza kujua taarifa zao na idadi yao. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe kwamba wajibu wetu kama serikali tutaendelea kuwaunganisha vizuri na kuona jumuiya zao kwa nchi walizo tunaendelea kuratibu vizuri kwa kupitia ofisi zetu za Ubalozi. Pia tunaendelea kuwashajihisha na kuwaomba kwamba pale walipo kila mmoja aendelee kuwa na hamu ya kutaka kurudi nyumbani ama kutoa taarifa zake, ili kuweza kuwatambua namna gani na kwa kiasi gani wanaweza kuishi na kufanya shughuli zao za maendeleo huko ughaibuni.

Swali la pili la kwamba lini na sherehe gani tunategemea kuifanya katika kuitangaza Sera ya *Diaspora.* Tutaandaa sherehe kubwa na itakuwa sherehe ya kuvutia kama yalivyo makongamano ambayo

tumekuwa tukiyafanya, ili kila mmoja wetu aweze kuona kwa kiasi gani sera yetu ya *diaspora* inakwenda mbele katika kushajihisha wenzetu kuja kushirikiana nasi katika harakati za maendeleo ya nchi yao ya asili.

Mhe. Spika: Mhe Hassan Khamis Hafidh kwa swali la nyongeza. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii na mimi kuuliza swali dhidi ya Wazanzibari muhimu sana wanaoishi nje ya nchi *diaspora*.

Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Awamu ya Saba, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa makusudi kwa uthubutu wake wa kuona umuhimu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwamba wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yao. Kwa hiyo, napenda sana kuchukua fursa hii kumpongeza kwa makusudi.

Lakini mbili Mhe. Spika, kwa kuweka *Hansard* sawa Idara ya *Diaspora* haiko miaka minne, ipo tangu Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein alipoingia madarakani. Lakini swali langu Mhe. Spika, Mhe. Rais Dkt. Shein amesema siku nyingi kwamba lazima tuwe na sera ili tuweze kuwaratibu vizuri Wanzanzibari wanaoishi nchi za nje, bado leo tunaambiwa sera itatangazwa mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, tangu alipoingia Rais Shein madarakani hiki ni kipindi kikubwa sana.

Swali langu je, ni lini Sera ya *Diaspora* itatangazwa na itaanza kutumika. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya

kuweza kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hassan Khamis Hafidh mwana *diaspora,* Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Welezo.

La kwanza Mhe. Spika, ndio hii faida ambayo tunasema ya kuwa na wataalam. Maana Mhe. Hassan Khamis Hafidh ni afisa wetu katika *Diaspora* na pengine Mwenyezi Mungu akitujaalia ataendelea kipindi chengine. Kwa hiyo, ataendelea kutusaidia katika Taasisi yetu ya *Diaspora* pindi atakapokuwa nje ya ulingo wa kisiasa. Lakini swali lake ni lini tutatangaza na itaanza kutumika Sera ya *Diaspora*.

Mhe. Spika, tumeeleza kwamba mwaka huu wa fedha unakwisha mwezi wa Juni na utaratibu wa Serikali inakwenda kwa mujibu wa mlichokipanga. Ninachomuomba tu Mhe. Mwakilishi asubiri kadi yake kwa ajili ya kwenda kusherehekea sherehe ya uzinduzi wa Sera yetu ya *Diaspora* na matumizi yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy swali la nyongeza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahim*. Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali la ziada lenye (a) na (b) Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutambua Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Swali langu:

a) Kwa kuwa wana *diaspora* ni Wazanzibari wanoishi nje. Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Zanzibar itawaruhusu Wazanzibari wale kuweza kumiliki nyumba na ardhi kihalali kabisa kama Wazanzibari wenyewe.

Kwa kuwa *ID* za Wazanzibari ni mamlaka au inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni lini *Diaspora* hawa na wao watapewa mamlaka ya kumiliki *ID* zao kama Wazanzibari. Kwa kuwa wao ni Wazanzibari na *ID* ya Zanzibar iko chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sio suala la Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chaani maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nadhani naweza kuyajibu yote mawili kwa pamoja. Tunapozungumza Mzanzibari kwa maana kwamba uraia wake unaendelea kuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwana *diaspora* ambaye hajapoteza sifa ya kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa na sifa za kuwa Mzanzibari Mkaazi ataendelea kupata haki na fursa zote kama tunazozipata sisi tuliopo nyumbani.

Lakini tunapokuja kwenye masuala ya haki ya raia sote tunajua kwamba nchi yetu haijakubali na hatujaruhusu mfumo wa uraia pacha. Kwa hiyo, tusitegemee mtu ambaye ana uraia wa nchi nyengine akahitaji kupata manufaa na fursa sawa sawa na raia wa Tanzania jambo hilo sheria zinakataza. Isipokuwa katika Sera hii ya *Diaspora* tulichokizingatia tunatambua wapo Wazanzibari ambao ni waumini wa dini ya kiislam wana haki ya kurithi mali kama walivyo wengine.

Sera hii inatengeneza utaratibu mzuri mtu ambaye atakuwa amepoteza sifa ya uraia wa Tanzania lakini ana haki ya kurithi kama warathi wengine aweze kupata haki yake na ndugu zake

waweze kupata haki yao. Kwa hiyo, sheria ya kupata Zanzibar *ID*, sheria ya kupata umiliki wa ardhi inakuhitaji kwamba uwe Mzanzibari Mkaazi na uwe na sifa ya mwananchi au raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini la ziada kwenye Zanzibar *ID* hata mgeni anapewa hatopewa kile kama cha Mzanzibari Mkaazi lakini atapewa kitambulisho ambacho kitamtambua kama yeye mwananchi aliyepo Zanzibar mwana *Diaspora* ana asili ya hapa na kama ana uraia pacha wa nchi nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Ali Suleiman Ali nimekuona kwa umuhimu wake hili swali naomba nikupe upendeleo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, mimi pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pia niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi wetu waliokuwepo nje ya Zanzibar au Tanzania.

Mhe. Spika mimi napenda kumuuliza swali dogo tu Mhe. Waziri. Pamoja na muda mrefu tumekaa tunasubiri sera lakini miaka minne mingi sana. Je, kwa hapa kati kati amepata ufumbuzi gani wa hao waliokuwa tayari kujitokeza kutusaidia Wazanzibari juu ya maendeleo mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali maarufu Shihata au mjomba au mshabiki wa Simba swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali hatujasubiri miaka minne, serikali tumeshaiandaa sera na katika kipindi cha miaka minne hii tumekuwa tukifanya makongamano. Makongamano hayo

yanaendelea kuturahisishia na kuimarisha daraja na mahusiano ya serikali baina ya Zanzibar, Tanzania na wenzetu wanaoishi ughaibuni. Katika kipindi chote hiki tokea kuanzishwa hii Idara ya *Diaspora* kumekuwa na michango na misaada mingi sana inayotoka kwa ndugu zetu walioko nje.

Skuli ya Unguja Ukuu wamesaidiwa, skuli zilioko mjini zimesaidiwa, Hospitali ya Mnazi Mmoja imesaidiwa, lakini pia wao wenyewe walio madaktari wa Tanzania wanaoishi Marekani wamekuja karibu mara tatu kutoa tiba, kutoa mafunzo na kutoa mchango wa taaluma yao kwa kuwasaidia Watanzania na Wanzanzibari wenzao waliopo hapa nyumbani.

Kwa hiyo, imani yangu kwamba Watanzania hawa *diaspora* wataendelea kutuchangia kadri siku zinapokuja. Kwa maana hiyo, serikali kuona kwamba daraja hili linaimarika kuweza kuleta tija kwa sote tuliopo nyumbani lakini na wao walioko ughaibuni.

Mhe. Spika: Waheshimiwa swali linalofuata la Wizara hii hii linaulizwa tena na Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chumbuni.

Nam. 6

Mafanikio Yaliyopatikana katika Mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa - Aliuliza:

Katika mwezi wa Septemba, 2016 kumefanyika mikutano ya Mawaziri na Marais wa Afrika Mashariki *(EAC)* na viongozi wetu wameshiriki kwenye mikutano hiyo.

a) Je, ni mambo gani mazuri ya kimaendeleo yaliyozungumzwa na kufanyiwa maamuzi yatakayoisaidia nchi yetu hasa Zanzibar.

b) Kuna fursa gani ambazo wananchi wetu watafaidika nazo zilizotokana na mikutano hiyo.

c) Serikali inachukua hatua gani ya kuwafikishia wananchi wake taarifa muhimu za kimaendeleo zinazopatikana kwenye vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chumbuni swali lake Nam. 6 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 8 Septemba, 2016 ulikuwa ni mkutano wa dharura ambao agenda zake zilikuwa ni kama ifuatavyo:-

   i) Agenda ya kwanza ilikuwa ni Kupokea Taarifa ya Majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kwa maana kwamba *(EPA) Economic Partnership Agreement;*

   ii) Agenda ya pili ilikuwa taarifa ya mazungumzo ya Amani ya nchi ya Burudi;

iii) Agenda ya tatu ilikuwa ni Kuridhia Mkataba wa Kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* kwa nchi ya Sudan ya Kusini; na

iv) Agenda ya nne ilikuwa ni Kuteuliwa na Kuapishwa kwa Naibu Katibu Mkuu Mpya wa Jumuiya ambaye alikuwa anatokea kutoka nchi ya Rwanda.

Mhe. Spika, agenda hizo zote zilikuwa ni muendelezo wa mambo mazuri ya kimaendeleo katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kama tunavyokumbuka kuwa katika mkutano huo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisisitiza msimamo wake wa kutoharakisha kusaini kwa mkataba wa *EPA* kwani umeonekana kuwa utaathiri maendeleo ya viwanda hapa nchini. Aidha, katika mazungumzo ya amani ya Burundi ambayo mpatanishi wake ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa yamekuwa na faida kubwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani maendeleo na usalama wetu hautokuwa imara bila ya kuwepo amani kwa nchi za jirani yetu. Vile vile, kujiunga kwa nchi ya Jamhuri ya Sudan ya Kusini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni faida kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani kunaongeza fursa za soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo sasa litakuwa limefikia watu takriban milioni 173.

b) Mhe. Spika, kuna fursa mbali mbali ambazo wananchi wa Zanzibar wanafaidika na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuzitaja chache ni pamoja na kubadilishana utaalamu katika sekta za elimu, afya, nishati na mazingira kwa nchi wanachama; kuwepo Makao Makuu ya Kamisheni ya

Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hapa Zanzibar ambayo yamesaidia kukuza na kuitangaza lugha ya Kiswahili duniani, utalii pamoja na ajira. Hivi karibuni lilifanyika Kongamano kubwa la matumizi ya lugha ya Kiswahili hapa Zanzibar ambapo wataalamu mbali mbali kutoka nchi wanachama walishiriki. Aidha, wajasiriamali wadogo wadogo wa Zanzibar wanafaidika na soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuuza na kutangaza bidhaa zao. Hivi karibuni, wajasiriamali wapatao 33 wa Zanzibar waliungana na wenzao wa Jumuiya ya Afrika Mashariki huko Burundi katika maonesho ya Juakali Nguvu Kazi.

c) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kutoa elimu ya masuala ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zinazopatikana katika maeneo mbali mbali. Elimu hiyo imetolewa kwa wajasiriamali, wafanyabiashara na makundi mengine ya wananchi katika Mikoa na Wilaya zote za Zanzibar. Elimu hiyo imeleta muamko kwa Wazanzibari kulitumia soko la Afrika Mashariki.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana *brother* wangu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa majibu mazuri na mwanana ambayo yanaleta matumaini sana katika uongozi wa serikali yetu.

a) Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kama utaratibu wa mikutano ya *EAC* kila mwaka inafanyika maana nakusudia 2016 umeleta mambo mazuri, lakini na 2017 pia hii mikutano ya *EAC* ilifanyika na sisi tulihudhuria. Je, kwa mwaka wa fedha 2017 mkutano huo ulijadili mambo gani ambayo ni muhimu na faida kwa nchi yetu.

b) Hayo mambo yaliyofanyika katika mkutano huo wa 2017 Wizara yako imefanya jitihada gani ya kuwafikishia wananchi yale mambo ambayo moja kwa moja yanakuwa ni fursa kwao wao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika tumesema kwamba Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ina kalenda yake unapozungumzia ile Mikutano ya *Summit*, Mikutano ya Baraza la Mawaziri na Mikutano ya Ngazi ya Wataalam.

Mkutano wa mwaka 2016 ulikuwa mkutano maalum na ndio maana ulikuwa umebeba agenda maalum, agenda zake kama tulivyozieleza kulikuwa na tatizo la *pressure* la Nchi za Magharibi hasa za Ulaya kutaka kuiharakisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuingia katika mkataba wa *EPA.*

Kwa hiyo, Jumuiya ikaona hatuwezi kwenda nchi moja moja lazima twende kwenye *block* na ili twende kwenye *block* lazima tufanye maamuzi kwa pamoja. Sote tunavyojua uamuzi wa *East African Community (EAC)* siku zote ni *confessor* kwa maana kwamba wanachama wote wakubali ndio mnafikia maamuzi. Kwa hiyo, utaratibu wa mkutano huu ulikuwa mkutano maalum na agenda maalum. Ratiba ya Mkutano wa *Summit* wa kawaida unategemewa kufanyika mwaka huu nchini Uganda. Agenda za mkutano zinaendelea, ninaamini tarehe 8 na 9 mawaziri wetu wanakwenda kuzungumzia masuala ya rasilimali zisizohamishika pamoja na mazingira ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya agenda.

Tarehe 27, 28 na 29 tutakutana tena Uganda kwa ajili ya Baraza la Mawaziri kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa *Summit*.

Kwa hiyo, manufaa watakayoyapata Serikali ya Zanzibar na wananchi wa Zanzibar yatatokana na agenda za mkutano utakuwa unahitimishwa kwa kikao cha mwisho cha *Summit* ambacho kinatarajiwa kufanyika Munyonyo nchini Uganda.

Mhe. Spika: Katibu Wizara inayofuata.

Nam. 7

Kutokuridhiwa kwa Mkataba wa *Maritime Labour Convention*

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa kutoridhiwa kwa baadhi ya Mikataba ya Kimataifa kama vile *Maritime Labour Convention* ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoleta vikwazo katika sekta ya usafiri wa baharini kwa hapa Zanzibar. Kwa kutilia maanani kwamba njia kuu ya usafiri kwa wakaazi wa visiwani kote ulimwenguni ni usafiri wa vyombo vya baharini ambavyo ndio kiunganishi kwa shughuli za kila siku katika maisha yao.

a) Je, Wizara imeshabaini nini chanzo hasa kinachosababisha kutoridhiwa kwa *Maritime Labour Convention.*

b) Kama wameshabaini, ni juhudi gani za makusudi zilizochukuliwa na Wizara kuhakikisha kwamba changamoto kama hii inapatiwa ufumbuzi wa haraka na wa kudumu ili kuhakikisha kwamba masuala kama haya hayaendelei kutokea kila mara.

c) Je, ni lini tatizo la kutoridhiwa kwa mkataba wa *Maritime Labour Convention* litamalizika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usarifirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Konde swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuchelewa kutoridhiwa kwa baadhi ya Mikataba ya Kimataifa kama vile *Maritime Labour Convention* ni moja kati ya changamoto inayoikabili sekta ya usafiri hapa Zanzibar. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini imefuatilia suala hili kwa karibu kwa kushirikiana na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini yaani *SUMATRA.* Ama kuhusu jambo lililokuwa likikwamisha kuridhiwa kwa mkataba huo ni kuchelewa kukamilika kwa taratibu za kawaida za kiofisi kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo.

b) Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia *ZMA* itaendelea kufanyakazi kwa karibu na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan katika mambo ya Muungano, ili kuhakikisha kuwa tunatumia fursa kwa pamoja za kutatua changamoto kama hizo mapema iwezekanavyo.

c) Kwa sasa napenda kulieleza Baraza lako tukufu kuwa changamoto hizo zinaendelea kutatuliwa na tayari Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshasaini mkataba huo yaani *Maritime Labour Convention.* Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa utekelezaji ambao ulikuwa ni chagamoto na sasa limetatuliwa. Lakini naomba kwa kuwa mkataba huu umeshafungwa kutoka na kumalizika hizo changamoto ambazo zilikuwa zinagusa sehemu zote mbili. Na kwa sababu Waziri amejibu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshasaini mkataba huo bila shaka itakuwa imesaini kwa niaba ya pande zote mbili na itakuwa kuna mambo ambayo yameshafikiwa vizuri.

a) Lakini swali langu lilikuwa nataka nijue. Je, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Zanzibar ambayo inahusika na maswali ya usafiri wa baharini kwa upande wetu sisi, Zanzibar ilishirikishwa vipi katika kutia saini mkataba huo wa *Maritime.*

b) Je, kusainiwa kwa mkataba huo ambao sasa tayari utekelezaji wake utaanza mara moja kwa upande wetu, sisi Zanzibar tutakuwa tunafaidika nini kutokana na kusainiwa kwa mkataba huo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawawiliano na Usafirishaji napenda kuchukua fursa hii kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nataka kumuarifu kwamba zoezi hili tumeshirikishwa tokea hatua za mwanzo. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Kamati yetu ya Baraza la Wawakilishi ya Ardhi na Mawasiliano nao walikuwa moja wapo ya kulisukuma hili suala na tulikuwa pamoja mpaka tukafanikiwa. Kwa hiyo, tumeshiriki kikamilifu na hadi kuridhiwa katika Bunge letu tukufu kipindi kilichopita cha 2017.

Lakini swali la pili ameuliza Zanzibar imenufaika vipi. Kwanza tulikuwa tunapata matatizo wale mabaharia wetu wanapokwenda katika meli wakifika baadhi ya nchi walikuwa hawawezi kutoka pale, lakini hivi sasa baada ya kuridhiwa mkataba huu kwa sababu inaonekana mabaharia wetu wanafuata mikataba yote ile ya wafanyakazi wanaruhusiwa kupita. Vile vile kulikuwa na baadhi ya *flag* kama *Panama* na nyengine walikuwa tabu kuwachukua mabaharia wetu. Kwa hiyo, kusema la ukweli tumefaidika sana na mkataba huu na kusema kweli tuwapongeze sana Kamati ya Ardhi na Mawasiliano katika hilo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali langu la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa mara baada ya ajali kubwa iliyoleta msiba mkubwa hapa Zanzibar, serikali ilisitisha safari za meli kwenda usiku Unguja na Pemba. Na kwa kuwa sasa tayari safari hizi zimeanza kwenda Unguja na Pemba wakati wa usiku. Je, serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha usalama wa abiria hao wa wananchi wake.

b) Je, serikali kwa nini haitoi amri au kuwaomba wawekezaji waliopo Zanzibar kuweza kupeleka boti za mwendo kasi Pemba ili kupunguza wimbi la abiria ambao wamekuwa

wengi sana hadi hapo meli zetu zitakapoanza kufanya kazi hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri ni swali jipya lakini nitakuruhusu ujibu inaonekana majibu unayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, ni kweli tulikuwa baadhi ya wakati meli hasa zinazokwenda Pemba ilikuwa hazituruhusu kwenda usiku kutokana na sababu maalum. Lakini hivi sasa baada ya yale masharti yote tuliyowawekea watu wa Azam pamoja na watu wa Shirika la Meli, hivi sasa ndio maana unazikuta meli zinakwenda usiku na sisi tumejipanga vizuri sana kuhakikisha kwamba zile taratibu zinazotakiwa za kiusalama hadi kusafirisha abiria kuwemo kwa kitu kinachoitwa *GSP* zinafanyiwa kazi na kwa kiasi fulani meli zile zinavyo hivyo vyombo ambavyo wanaweza kuwasiliana na sisi wakati wowote.

Mhe. Spika, swali lake la pili kuhusu kupeleka vyombo vya haraka kama *speed boat* kwenda Pemba. Mhe. Spika, napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba bahari ya kutoka Unguja kwenda Pemba ni bahari ambayo inakuwa baadhi ya wakati inachafuka hasa kutokana na mkondo wa Nungwi. Hata hivyo, kuna vyombo ambavyo vya mwendo kasi lakini kutokana na *speed* na mkondo wa bahari ambavyo vimekuwa vinafanya kazi sasa hivi kama hiyo *Azam Sealink* lakini sio kwa mwendo kasi unaotakiwa. Sisi tunaendelea kuwashajihisha wananchi, wawekezaji kuendelea kutumia fursa hiyo kwa kuleta vyombo vinavyokwenda kwa mwendo kasi. Kama nilivyosema tunataka

vyombo ambavyo vitakuwa vina gharama kubwa na vile vile vyombo ambavyo tumeona *MS. Sepideh* ilipokuwepo kabla, ni vyombo ambavyo bahari yake inatakiwa iwe ni yenye kustahamili mkondo ule. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 16

Kutangazwa Kiutalii Maeneo ya Kihistoria yaliyopo Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Katika Sekta ya Utalii Zanzibar Kisiwa cha Unguja kimepata ukuaji mzuri na ufanisi lakini kwa upande wa Pemba vipo vivutio vingi ambavyo watalii wangependa kuviona na kuitangaza Zanzibar Kimataifa. Hata hivyo, kuna changamoto ambazo bado wizara inatakiwa izipe kipaumbele na jitihada za makusudi za kukuza utalii katika Kisiwa cha Pemba.

(a) Je, wizara imechukua hatua gani kuvitangaza vivutio na maeneo ya kihistoria yaliyoko Pemba ndani ya Zanzibar na duniani kiutalii.

(b) Je, msitu wa Ngezi uliopo huko Pemba na misitu mengine ya hifadhi imetangazwa kiutalii.

(c) Je, ni aina gani ya wanyama wa asili pamoja na vivutio vilivyomo ndani ya msitu wa Ngezi kiutalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu**:**

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nakiri ni kweli kuna maendeleo makubwa ya sekta ya utalii Kisiwani Unguja ukilinganisha na Kisiwa cha Pemba. Hali hiyo imetokana na sababu tofauti ikiwemo wawekezaji wengi kushajihika kuwekeza katika Kisiwa cha Unguja na uhaba wa miundombinu ikiwemo Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake.

(a) Mhe. Spika, njia zinazotumiwa na Kamisheni katika kutangaza vivutio vyake ni kuviweka katika majarida ya matangazo yanayotayarishwa na Kamisheni pamoja na kuwapeleka wapiga picha na waandishi wa majarida ya utalii kuvitembelea vivutio hivyo pale wanapokuwa nchini.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia Kamisheni ya Utalii inautangaza msitu wa Ngezi kama ni kivutio cha utalii. Matangazo hayo hufanyika kupitia majarida mbali mbali yanayotayarishwa na Kamisheni, mtandao wa Kamisheni ya Utalii na *DVD* za kutangazia utalii zinazotayarishwa na Kamisheni.

(c) Mhe. Spika, vivutio vilivyopo katika msitu wa Ngezi ni pamoja na popo, ndege, miti inayotumika kwa dawa, mabaki ya kiwanda cha mbao kilichokuwa kikifanya kazi miaka ya 1960. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, na mimi nimpe pongezi Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina nyongeza ya swali (a) na (b).

a) Katika msitu wa Ngezi kuna barabara kubwa inayokwenda Mkia wa Ng'ombe, Vumawimbi na Kigomasha. Kwa hivyo, njia ile imepita kati kati na njia ile kwa tafsiri ni kwamba haitotiwa lami na ina mashimo mabaya sana. Je, jambo la kwanza serikali haijulikani mtu gani anakwenda *tour* na mtu gani anapita njia, hivyo haioni serikali inapoteza mapato.

b) Pamoja na kwamba kuna vivutio vingi vya popo, ndege na kila kitu, katika msitu wa Ngezi kuna makaburi mawili ambayo huwa yameandikwa kitaaluma fulani na yana historia fulani. Je, Mhe. Naibu Waziri unaweza kutueleza historia fupi ya makaburi yale ili kupata uhakika wa wale watu wanaokwenda wakiganga au kuchukua fani yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi lenye kipengele (a) na (b) yote kwa pamoja.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika msitu ule au barabara ile kuna barabara ambazo zimegawika kwenda vijiji ambavyo amevitaja Mhe. Mwakilishi. Mhe. Spika, kwa kuwa tuna Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi msitu ule hauruhusiwi kukatwa kwa ajili ya kujenga barabara ile kwa utiaji wa lami, kwani tutakapoweka lami kuna miti tunaweza tukaipoteza kutokana na lami ile au athari za kutiwa lami.

Mhe. Spika, pia katika makaburi yale yaliyopo kwenye msitu ule historia yake inaonekana kwamba wakati ambao wakoloni walikuwa wanakuja katika nchi yetu ya Zanzibar wazee wale wao walijitokeza na kuomba kwa Mwenyezi Mungu wasikutane na wakoloni wale, kwa taarifa ambazo nimezifanyia utafiti. Kwa hiyo, watu wale walipita katika msitu ule na hatimae wakazama pale na zikaonekana nguo zao tu, hivyo watu wakaanza kufanya utafiti baada ya kuonekana ncha ya nguo zao wakaona watu wale wameingia pale na wakoloni hawakukutana nao wakati wameingia nchini. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza kwa Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, serikali ilikuwa na dhamira kubwa ya kujenga barabara ambayo alielezea Mhe. Mwakilishi inayoanzia pale mwanzoni mwa msitu mpaka mwisho kule. Lakini kutokana na wana mazingira na watu mbali mbali wanaoamini utunzaji wa uoto wa asili walijitokeza sana kuishauri serikali kwamba eneo lile tusiweke barabara yenye lami. Kama mnavyokumbuka wakati wa mheshimiwa aliyekuwa Mwakilishi wa Konde ambaye amefariki dunia Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema peponi, aliitetea sana barabara ile. Lakini suala la kimazingira liliheshimiwa na ndio maana mpaka leo serikali inachokifanya kila inapotokea uharibifu katika eneo lile hujaza kifusi na kuifanyia utaratibu wa kawaida, lakini si kuweka lami. Hiyo inatokana na mambo ya kimazingira kama ambavyo Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwa upana wake.

Hata hivyo, kuhusu kaburi la pale ndani ameelezea vizuri na pale ukifika yapo maelezo yake yameandikwa. Kwa hivyo, watu ambao wanahitaji kujua historia ningependa tu kutoa wito kwa

viongozi na wananchi mbali mbali kwamba waende watembelee msitu ule na historia yake imeandikwa watapata kila liliomo pale ndani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake amejikita sana katika televisheni na *DVD*, wakati wenzetu wanapotangaza vivutio na utalii wao wanatangaza katika ndege zinazokwenda nchi za nje. Je, wizara yako imejipanga vipi ili kuona Zanzibar na sisi tunajitangaza katika ndege zinazokwenda nchi za nje. Vile vile vivutio hivyo mnakuwa mkitumia lugha gani badala ya lugha yetu ya Kiswahili ili kuona watalii wanavutiwa sana na utalii wetu wa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi. Mhe. Spika, kwa sasa hivi tumeshaanza mazungumzo na baadhi ya Mashirika ya Ndege ili kuona utalii na vivutio vyetu tunavitangaza kutoka nchi mbali mbali, Mashirika ambayo tumeanza kuzungumza nayo na kwa kuwa hii ni biashara mpaka tukubaliane. Tumeanza na Shirika la Comoro, *Air Tanzania* na Ethiopia, wakati tutakapokubaliana tutaendelea kutangaza vivutio vyetu na utalii katika mashirika ya ndege mbali mbali.

Mhe. Spika, vile vile kwa upande wa lugha ambazo tunazitumia katika utangazaji huu, tunatumia lugha tofauti ukiacha lugha yetu ya Kiswahili, tunatangaza kwa lugha za zile nchi ambazo wanazizungumza. Kwa mfano, kuna Shirika la Anhui ambalo ni la China hawa wanatutangazia kwa lugha yao ya Kichina, lakini kwa bahati nzuri tu juzi tulikuwa na Balozi wa Israel pia tulifanya nae

mazungumzo na akatwambia kwamba atatangaza au atakaa na sisi ili kuona ametafsiri kwa lugha ya Kiisraeli ili utalii wetu utangazike vizuri kwa lugha za nchi ambazo wanazitumia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ningependa kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kama alivyosema katika majibu yake mama kwamba wawekezaji wengi sana wamejichomoza kwa upande wa Unguja, lakini ukiangalia na Pemba sasa hivi wawekezaji wengi sana wamepata mwamko na kuwekeza katika maeneo mbali mbali ambapo kuna mahoteli makubwa ya kitalii mengi na mazuri sana. Je, Mhe. Waziri kupitia wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji mtashirikiana vipi angalau kuweka miundombinu ya barabara katika maeneo yale ili yaweze kufikika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kama alivyokiri na yeye kwamba katika jibu langu mama nimesema watalii wengi au wawekezaji wengi wameshajihisha kuwekeza katika kisiwa cha Unguja ukilinganisha na kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, lakini nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba sisi pamoja na Wizara ya Ujenzi lakini barabara zile za ndani mara nyingi wanaojenga ni Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Nimhakikishie tu kwamba tutashirikiana kwa pamoja ili barabara zile zipitike. Kwa sababu sasa hivi pia tuna mpango wa kuweka kifusi kama alivyoelezea Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili tuone wageni wetu wanafika kule bila ya kadhia yoyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya upendeleo kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza (a) nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye kuvutia, lakini ningependa kumuuliza swali la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri katika majibu yake mama ametwambia kwamba, vivutio vile huwa wanavitangaza kwa hapa kwetu yaani kwa kwenda wanafunzi au katika vijarida na kwenda upiga picha. Je, Mhe. Naibu Waziri anahisi kwamba hivi vivutio alivyosema kwamba vinatangazwa kwa kupigwa picha na kwenda wanafunzi kutembelea anahisi vinakidhi haja. Kama havikidhi haja je, kuna taratibu gani ambazo wameziandaa ili kuviimarisha, kuviboresha vivutio hivi wale wageni wetu wanapofika hapa wazidi kwenda kuvitembelea ili pato la nchi yetu liongezeke.

(b) Kwa kuwa tunaona kwamba vivutio hivi katika Unguja pia kwa sababu Mhe. Suleiman Sarahan Said ameulizia kuhusu Pemba, lakini hata hapa Unguja hatujaona zile mishemishe hasa zinazohusiana na kuviimarisha vivutio hivi katika suala la utalii. Je, wizara imeandaa miundombinu gani au imeandaa taratibu gani kuweka maonesho au viburudisho vya kila aina katika maeneo haya ili wale watalii wazidi kupata nguvu na moyo wa kwenda kuyatembelea maeneo haya. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) vyote kwa pamoja kama ifuatavyo.
Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna haja ya kuweka utaratibu katika kuviboresha vivutio hivi. Lakini hatua ambayo tumekuwa tukichukua wizara kuna vipindi maalum kama nilivyoeleza

ambavyo tumetayarisha kupitia televisheni hasa kwa faida ya Wazanzibari. Kuna vipindi ambavyo tumeviweka kuna "Hazina Iliyojificha", kipindi hiki naomba sana Waheshimiwa wafuatilie kinatoka Jumatatu saa 3:00 Usiku, lakini marudio yanakuwa ni siku ya Jumane wakati wa saa 6:00 mchana.

Hili nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba na yeye awe tayari kufuatilia taarifa hizi ili aone utaratibu wa vituo vyetu na utalii jinsi tunavyotangaza kwa wananchi wetu lakini na kwa wanafunzi pia.

Vile vile utaratibu ambao wizara umeuweka pia kwa upande wa wanafunzi au kwa upande wa Zanzibar, pia bado niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, kuna matamasha ambayo tumekuwa tukiyaandaa. Leo hii kuna Tamasha la Utamaduni au la Sauti ya Busara naomba Mheshimiwa pale tunapata watalii, tunapata wageni mbali mbali. Lakini na Waheshimiwa Wawakilishi nawakaribisha sana, tuungane pamoja kwenda kwenye matamasha haya ili tuone jinsi watalii wanavyoshajihika na kufurahia matamasha yetu na maandalizi yetu jinsi tulivyoyaandaa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante wakati wa maswali umekwisha. Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya wageni kwanza, wageni waliopo ni wageni wa Spika na wanatoka katika Ofisi ya Pamoja Zanzibar jumla yao ni watano na ni ofisi ambayo ni sehemu ya Chuo chetu cha Ufundi cha Karume. Wa kwanza ni Ndugu Gernoth Erich Klug ambaye ni Mkurugenzi Mkuu, wa pili ni Ndugu Daud Mahfoudh Awesi ambaye ni Fundi Mkuu, wa tatu ni Ndugu Ramadhan Mussa Mohammed ambaye ni Meneja wa Ofisi, wa nne ni Bwana Khamis Hassan Khamis ambaye ni Mlezi Msaidizi wa Wanafunzi na mwisho ni Ndugu Mtumwa Suleiman Nassor ambaye ni Karani Mkuu.

Karibuni sana, karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe, mtaona kwamba kwenye *order paper* yetu baada ya shughuli hii tutakuwa tumemaliza shughuli za siku ya leo na mtakumbuka kwamba tulikubaliana tutakuwa na semina mara baada ya kumalizika kwa kipindi hiki cha maswali. Kwa hiyo, semina hiyo ipo na tumepanga kwamba tutafanya halafu *lunch* tutapata hapa hapa na baadae tutaendelea kumalizia kutokana na umuhimu wa shughuli yenyewe hii ya semina. Kwa hiyo, baada ya kutoa matangazo haya naomba sasa niakhirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka kesho siku ya Ijumaa saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 4:01 Baraza liliakhirishwa hadi siku ya Ijumaa Tarehe 09/02/2018 saa 3:00 asubuhi)